Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto

ICPC ni nini na kwa nini itekelezwe?

Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto (International Child Protection Certificate – ICPC) kimeundwa kwa ari ya pamoja kati ya Shirika la Taifa la Jinai (NCA) na Ofisi ya Kumbukumbu za Jinai ya ACRO. Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinasaidia kulinda watoto nje ya Uingereza dhidi ya tishio la raia au watu walioishi Uingereza ambao wanafunga safari, ili kuweza kufikia watoto walio katika hali ya unyonge kwa nia ya kuwadhuru. Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinasaidia kulinda watoto dhidi ya watu hao wenye hatari ya kuwabaka, kuwadhuru kimwili, kuwadhuru kisakolojia na/au kutowajali. Wahalifu hawa hutafuta uhusiano wa moja kwa moja na watoto kwa kupitia ajira, kazi za kujitolea na za hisani. Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kimesanifiwa ili kuwazuia kuweza kufanya hivyo.

Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto ni uchunguzi wa kumbukumbu za jinai katika hifadhidata za polisi na usalama wa taifa za Uingereza. Kinaweza kuombwa na mashirika kwa raia wote wa Uingereza (pamoja na raia wasio wa Uingereza waliowahi kuishi Uingereza) ambao wanatafuta kazi nje ya Uingereza zinazohusika na watoto. Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinaweza pia kuombwa na watu ambao tayari wameajiriwa na wanafanya kazi na watoto.

Kinapotumika pamoja na taratibu makinifu za kulinda usalama ambazo tayari zipo, Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinawezesha mashule na mashirika mengine yaliyo nje ya Uingereza kuweza kuchufanya maamuzi yakiwa na taarifa kamili, yanayoweza kuleta madhara, kuhusu watu yanaowaajiri yajue kama wanafaa kufanya kazi na watoto.

Kwa kujumuisha Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto ndani ya mchakato wako wa kuajiri, utaongeza ulinzi wa usalama wa ziada kwenye taratibu zilizopo na kuchukuwa hatua muhimu katika kusaidia kulinda watoto dhidi ya watu wenye nia ya kuwafanyia ukatili na kuwaonea.

Cheti kitaonyesha nini?

Cheti kitakuwa na data za hukumu za jinai kwa uhalifu uliofanywa Uingereza, na kinaweza pia kuwa na taarifa za hukumu ya makosa ya jinai yaliyofanywa katika nchi ambazo taarifa kama hizo zimefichuliwa Uingereza kwa kupitia mifumo ya kubadilishana iliyopo. Aidha, ikiwa kama sehemu ya mchakato wa Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto, NCA itafanya tathmini ya habari za upelelezi, na taarifa zinazopatikana na kuziweka kwenye cheti zozote inazoona zinahusika katika maslahi ya kulinda mtoto.

Cheti kina sehemu mbili:

- Sehemu ya 1 – Kufichua taarifa zozote zilizo kwenye hifadhidata za polisi wa Uingereza za hukumu, mashtaka yanayosubiri kupelekwa mahakamani, ilani, onyo, tahadhari na upelelezi unaoendelea, kufuatana na muundo wa ACRO step-down model.

- Sehemu ya 2 – Kujumuisha taarifa zilizotathmininiwa kuwa zinahusika na kustahili kufichuliwa na NCA ili kuonyesha hatari iletwayo na mwombaji kwa watoto au vijana wadogo.

MUHIMU: Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto hakionyeshi ufao wa mwombaji kufanya kazi na watoto. Badala yake, kitumike kama nyezo ya ziada, pamoja na vipengele vingine vya kawaida vya shirika vya kulinda usalama ambavyo mwajiri atumie ili kufanya maamuzi yanayozingatia taarifa kamili.

Shule na mashirika mengine vinatekelezaje Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto?

Ili kuweza kufikia mchakato wa Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto, shirika lazima litimize vipengele vifuatavyo:

- lifanye kazi zinazohusu watoto;
- ajiri wafanyakazi wa kulipwa au kujitolea kutoka Uingereza, ikiwemo pamoja na watu ambao waliishi Uingereza awali;
- lisiwe na uhusiano rasmi na Uingereza na uwezo wa kufikia Huduma ya Ufichuzi na Uzuizi (Disclosure and Barring Service - DBS).

Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinalipiwa na mtu anaetafuta kazi. Kwa maelezo zaidi juu ya bei, tafadhali tembelea www.acro.police.uk/icpc. Vyeti vinaweza kutolewa kwa ombi la mwomba kazi tu; mwajiri hawezi kuomba kwa niaba yake. Inashauriwa kwamba mashirika yahimize wafanyakazi kuwasilisha Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kwa kukifanya kiwe sehemu ya lazima katika uchunguzi unaofanywa kabla ya kuajiriwa. Wafanyakazi waliopo wanaweza kuombwa kwa vipindi kutoa Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto ikiwa sehemu inayoendelea ya mchakato wa kuhakiki.

Kama mwajiri angependa kumuomba mtu atoe Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto, anaweza kumwagiza atembelee tovuti ya ACRO (www.acro.police.uk/icpc) ili kukamilisha kujaza fomu ya maombi. Mwongozo juu ya mchakato huu unapatikana kwenye tovuti.

Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kinaonyesha taarifa zilizowekwa kwenye hifadhidata za polisi na usalama wa taifa wakati wa kutoa cheti; hivyo hukumu zozote zilizowekwa baada ya tarehe hii hazitaonyeshwa. Ni juu ya mwajiri kuamua kwa mrudio gani wafanyakari wanapaswa kuleta upya Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto.

Mashirika yanaweza kuwasilisha maombi kwa niaba ya wafanyakazi, lakini fomu lazima ijazwe na kusainiwa na mwombaji mwenyewe. Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto kitatolewa moja kwa moja kwa mwombaji; hakiwezi kutumwa kwenye shirika.

Tafadhali zingatia kwamba mashirika yaliyo nje ya Uingereza ambayo yanaufikivu wa ukaguzi wa DBS hayana uwezo wa kushauri waajiriwa wapya au waliokuwepo kupata Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto . Njia za kawaida za kufanya maombi kwa kupitia kwenye DBS zitatumika kwenye hali kama hizi.

Kwa taarifa zaidi juu ya Cheti cha Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Mtoto, tafadhali tembelea: www.acro.police.uk/icpc.